BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAOMBI YA UDAHILI KWA WAOMBAJI WA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo katika Vyuo ambavyo si Vyuo Vikuu ama Vyuo Vikuu Vishiriki nchini. Jukumu mojawapo la Baraza, ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Ufundi nchini yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Baraza linapenda kuufahamisha umma kuwa **Udahili** wa wanafunzi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa kozi/programu zote **isipokuwa Ualimu** umefunguliwa rasmi kuanzia tarehe **28 Mei, 2019** na utaendelea **hadi Tarehe 2 Septemba, 2019** kwa Vyuo vyote vinavyotoa mafunzo katika ngazi hizo.

Kwa waombaji wa **programu za Afya** katika **Vyuo vya Serikali** watatakiwa ama kuomba moja kwa moja kupitia vyuoni ambako vyuo vitawasajili kupitia *'Instititutional Panel'* ya chuo husika au wanaweza kuomba kupitia tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) (www.nacte.go.tz) kwa kubofya kwenye *'Apply online (SAVS)'* kisha kufuata maelekezo.

Kwa waombaji wa programu za Afya kwenye **Vyuo visivyo vya Serikali na waombaji wa programu nyingine zote** watatakiwa kuomba moja kwa moja kwenye vyuo husika. Hivyo vyuo vitapokea maombi na kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenye sifa na kisha kuwasilisha NACTE majina ya waliochaguliwa kwa **njia ya mtandao** kwa ajili ya uhakiki kabla ya kuyatangaza. Vyuo vinaelekezwa kuzingatia utaratibu wa udahili kama ulivyotolewa na Baraza katika masomo 2017/18.

Hivyo wahitimu wote wa Elimu ya Sekondari na Vyuo wenye sifa za kujiunga na kozi za Astashahada na Stashahada, wanashauriwa kufanya maombi kwa umakini ili kuweza kupata nafasi ya kujiunga programu wanazozipenda na ambazo wanatimiza vigezo/sifa za kujiunga nazo kwa mwaka 2019/2020.

Aidha, Baraza linataarifu umma na vyuo kwamba udahili wa wanafunzi wapya katika programu ya **Cheti cha Msingi cha Huduma ya Afya Ngazi ya Jamii (Basic Technician Certificate in Community Health)** umesitishwa hadi hapo itakapo tangazwa tena.

Pia baraza linawashauri waombaji na wazazi kuhakikisha kuwa wanaomba kwenye Vyuo vinavyokidhi ubora ambavyo vimeorodheshwa kwenye **Kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa mwaka wa masomo 2019/2020 (Admission Guidebook for 2019/2020 Academic Year).**

Mwongozo wa Udahili unapatikana katika tovuti ya NACTE (**www.nacte.go.tz**).

IMETOLEWA NA:
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)
TAREHE: 28/05/2019